Jikinge, jilinde, Chukua Tahadhari

Februari

# TIRA Updates 2025

Kwa Soko Salama la Bima

Toleo No.03 | Jarida la Mtandaoni | www.tira.go.tz




## Uhakika wa Matibabu ni Kuwa na Bima ya Afya!

HALIUZWI

**Wasiliana nasi** coi@tira.go.tz | **Au tupigie** +255 222 132 537 | **FB, IG, X:** //@tira_tz

# Yaliyomo

01



08




01 Rais Mwinyi Apokea Taarifa ya Utendaji wa Soko, Aipongeza TIRA kwa Kuleta Mageuzi kwenye Sekta ya Bima

04 Wajumbe Bodi ya Taifa ya Bima Wanolewa Mada Mbalimbali Kuhusu Bima

06 Mabalozi wa Bima na Wadau wa Takaful nchini Wabadilishana Uzoefu

08 Mali na Miradi ya Serikali Ikatiwe Bima, Kupunguza Hasara za Majanga

10 FSD Africa na TIRA Washiriki Mkutano Kujadili Ukuzaji wa Sekta ya Bima Nchini na Uchumi

12 TIRA Yakutana na Wadau wa Bima Zanzibar Yajadili Uboreshaji wa Huduma TIRA

14 Mabenki Yahimizwa Kupunguza Ujira Gharama ya Bima iwe Rahisi

16 DC Chakechake Asisitiza Ushirikiano Sekta ya Bima

18 TIRA Yaendelea Kuhamasisha Utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote Mkoani Kigoma

20 Changamkieni Fursa Muwe Mawakala wa Bima – Dkt. Saqware

21 TIRA, POLISI Kutumia Mifumo ya Kuimarisha Usalama Barabarani

22 Kateni Bima za Afya, Gharama Nafuu Matibabu Bila Kikwazo

24 TIRA Yawezesha Waandishi wa Habari Njombe Kuripoti Taarifa za Bima kwa Ufanisi



**Jarida Hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma**

**Mhariri**
Hadija Maulid

**Waandishi**
Tabia Mchakama
Anna Massao

**Msanifu**
Abubakari W. Kafumba


TIRA Updates ni jarida la mtandaoni linaloandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, likilenga kutoa taarifa muhimu, kuelimisha, na kuhamasisha umma kuhusu sekta ya bima nchini. Jarida hili limeandaliwa ili kufikia wadau mbalimbali wa sekta, wakiwemo mawakala wa bima, kampuni za bima, watoa huduma na watumiaji wa bima.

Jarida la TIRAUpdates lina taarifa za matukio mbalimbali, ikijumuisha uzinduzi wa miradi mipya, semina, warsha za mafunzo, na mikutano muhimu inayofanyika ndani ya sekta ya bima.

Mbali na taarifa za matukio, TIRAUpdates lina makala maalumu zinazolenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima.

Aidha, toleo hili litaangazia matukio, habari na taarifa muhimu za mwezi Februari 2025.




Scan
Kusoma Kidijiti


Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe
**info@tira.go.tz**

Au
Piga simu bure **+255 222 132 537**

Tovuti yetu
**www.tira.go.tz**

# Rais Mwinyi Apokea Taarifa ya Utendaji wa Soko, Aipongeza TIRA kwa Kuleta Mageuzi kwenye Sekta ya Bima




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amepokea Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima ya Mwaka 2023 na kuipongeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kwa mchango wake mkubwa katika mageuzi ya sekta ya bima. Hafla hiyo ilifanyika Februari 20, 2025 katika Hoteli ya Verde, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, na kuhudhuriwa

na viongozi mbalimbali wa serikali na wadau wa sekta ya bima.

Katika hotuba yake, Dkt. Mwinyi alisisitiza umuhimu wa sekta ya bima kwenda sambamba na kasi ya serikali zote mbili kwa kutumia ubunifu na teknolojia ili kuongeza ufanisi. Alieleza kuwa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zina dhamira ya dhati ya kuendeleza sekta ya bima kama nyenzo ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Aidha, Rais Dkt. Mwinyi alihimiza kuongeza juhudi katika matumizi ya TEHAMA ili kuboresha huduma za bima na kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanafikiwa. Alisisitiza umuhimu wa kuimarisha utafiti wa vihatarishi ili kubuni bidhaa za bima zinazoendana na mahitaji ya soko, hususan kwa mali za serikali na sekta binafsi.

Dkt. Mwinyi alihimiza TIRA iendelee kupitia sheria na kanuni mbalimbali ili ziendane na mazingira ya sasa na ukuaji wa uchumi wa kidigitali. Alisema kuwa elimu kwa umma kuhusu bima ni nguzo muhimu kwa ukuaji wa sekta hiyo na hivyo ni lazima jitihada zaidi zifanyike ili kuongeza uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa bima.

Akiwasilisha taarifa hiyo Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware, alieleza kuwa TIRA itaendelea kuweka mazingira wezeshi katika soko la bima ili kuchochea ukuaji wa sekta hiyo na kuongeza mchango wake katika pato la taifa.

Aliongeza kuwa mamlaka imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na wadau wa bima ili kuhakikisha kunakuwa na bidhaa bora zaidi zinazoakisi mahitaji ya wananchi na taasisi mbalimbali.

Dkt. Saqware pia alibainisha kuwa TIRA imefanikiwa kupanua huduma zake kwa kufungua ofisi za kanda Unguja na Pemba, hatua inayolenga kuimarisha usimamizi wa sekta ya bima na kuwahudumia wananchi kwa karibu zaidi. Alisema mamlaka inazingatia mageuzi ya kidigitali kwa lengo la kuhakikisha huduma za bima zinapatikana kwa urahisi na kwa ufanisi zaidi.








NMB

# Wajumbe Bodi ya Taifa ya Bima Wanolewa Mada Mbalimbali Kuhusu Bima



Mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi ya Taifa ya Bima (NIB) yalifanyika Februari 19, 2025 katika ukumbi wa mikutano ZURA, Zanzibar Lengo likiwa ni kuongeza uelewa kwa wajumbe wa Bodi hiyo juu ya shughuli mbalimbali za Mamlaka. Mafunzo hayo yalihudhuriwa pia na viongozi wakuu wa Mamlaka, Menejimenti na baadhi ya watumishi.

Katika mafunzo hayo mada mbalimbali ziliwasilishwa zikiwemo mada kuhusu Skimu ya bima ya kilimo, Bima ya Afya kwa Wote na masuala ya hatifungani (bonds). Katika wasilisho la bima ya afya na kilimo lilizingatia namna ya utekelezaji wake, sheria zinazosimamia, kulindwa kwa walaji na masuala mengine muhimu.

Akifungua rasmi Mafunzo hayo Makamu Mwenyekiti wa Bodi Dkt. Suleiman Mohamed kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi hiyo CPA Moremi Marwa alisema mafunzo hayo kwao ni muhimu kwani ni fursa nzuri ya kujifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu maendeleo na utatuzi wa changamoto katika sekta ya bima.

Nae Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware amesema alieleza matarajio yake kuhusu mafunzo hayo ambapo alisema wajumbe wa Bodi wanahitaji kuwezeshwa kupata uelewa mpana kuhusu maswala mbalimbali ya bima ili waweze kuwa na michango chanya wakati wa kuishauri Mamlaka kuhusu utekelezaji wa mikakati na mipango hasa katika maeneo muhimu yanayogusa maisha ya watanzania wengi kwa kuwa michango hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya taasisi yetu na sekta kwa jumla.





# Mabalozi wa Bima na Wadau wa Takaful nchini Wabadilishana Uzoefu



Tarehe 20 Februari 2025- katika ukumbi wa IMTC BOSNIA-Zanzibar, Mabalozi wa Bima Nchini Mhandisi. Zena A. Said-Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhe. Japhet Hasunga-Mbunge, na Mhe. Wanu Hafidh-Mbunge walikutana na wadau wa Takaful Nchini kwa lengo la kubadilishana uzoefu wa biashara ya Takaful walioupata nchini Malyasia na kujadili namna ya utekelezaji wa miongozo mbalimbali ya Takaful nchini Tanzania.

Katika Kikao hicho, TIRA kupitia Kamishna wa Bima, (Dkt. Baghayo A. Saqware waliwasilisha Taarifa ya kazi mbalimbali zilizofanywa na mabalozi wa bima pamoja na Taarifa ya utekelezaji wa Mwongozo wa Takaful na mapendekezo ya namna bora ya kuendeleza biashara ya Takaful nchini Tanzania.

Takaful ni mfumo wa bima wa ushirikiano unaozingatia misingi ya Shariah, ambapo wanachama huchangia fedha kwa pamoja ili kusaidiana katika kukabiliana na hasara au majanga yanayoweza kutokea.

Mfumo huu unafuata kanuni za uwazi, uadilifu, mshikamano, na kuepuka mambo kama riba, gharar (kutokuwa na uhakika kupita kiasi), na maisir (kamari) katika shughuli zake. Pia, usimamizi wake hufanywa kwa kuzingatia mwongozo wa bodi ya Shariah ili kuhakikisha uendeshaji wake unakubalika kisheria.













# Mali na Miradi ya Serikali Ikatiwe Bima, Kupunguza Hasara za Majanga







Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware, ametoa rai kwa watumishi wa Mkoa wa Geita kuhakikisha kuwa mali na miradi mikubwa ya Serikali inakatiwa bima ili kupunguza hasara zinazoweza kutokea wakati wa majanga.

Dkt. Saqware amesema hayo leo, 28 Februari 2025, mkoani Geita katika ziara ya kutembelea mikoa mbalimbali, ikilenga kuhamasisha wakuu wa mikoa, makatibu tawala na watumishi wa umma kuhusu umuhimu wa bima. Ziara hiyo pia inalenga kuwaelimisha kuhusu fursa zilizopo katika sekta ya bima, ikiwa ni pamoja na kuwa mawakala wa bima na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

kifungua mkutano huo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, Bw. Mohamed Gombati, amewahimiza watumishi wa serikali kushiriki kikamilifu katika sekta ya bima na kuhakikisha miradi yote ya maendeleo inalindwa kupitia bima. "Serikali inawekeza kiasi kikubwa cha fedha katika miradi ya maendeleo, hivyo ni muhimu miradi hii ikakingwa na bima ili kuhakikisha inapata fidia pale majanga yanapotokea," alisema Bw. Gombati.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Usimamizi , Bw. Christopher Mapunda, amesema kuwa TIRA ina jukumu la kuhakikisha elimu ya bima inawafikia wananchi wengi zaidi ili kupanua wigo wa matumizi ya bima nchini. "Kuna haja ya kuendelea kutoa elimu kuhusu bima ili wananchi waone umuhimu wake

katika kulinda mali, maisha, uwekezaji na afya. TIRA itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha watanzania wengi zaidi wanapata uelewa wa bima na kunufaika na huduma zake," alisema Bw. Mapunda.

Ziara hii ni sehemu ya mkakati endelevu wa TIRA kuhakikisha bima inachukua nafasi kubwa katika maendeleo ya taifa kwa kulinda mali za umma na kuhakikisha wananchi wanakuwa na kinga dhidi ya majanga mbalimbali.





# FSD Africa na TIRA Washiriki Mkutano Kujadili Ukuzaji wa Sekta ya Bima



Mkutano kuhusu sekta ya bima nchini umefanyika Februari 04, 2025 jijini Dar es salaam, ukifunguliwa rasmi na Naibu Kamishna wa Bima Tanzania Bi. Khadija Said. Mkutano huo ambao uliandaliwa na FSD Africa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ulilenga kuwakutanisha wadau wa sekta hiyo kuangazia masuala ya Uchumi na bima na njia zitakazoweza kutumika na kuleta mazingira bora zaidi ya kiuchumi hasa kwa wananchi wa Tanzania na Africa kwa ujumla.

Bi. Khadija alitoa rai kwa washiriki mkutano huo kutumia jukwaa hilo kwa majadiliano yenye tija na kutafakari njia za kukuza Uchumi huku pia sekta ya bima ikijikita kutengeneza bidhaa mbalimbali zitakazoweza kudumu muda mrefu na zenye unafuu kwa wananchi, ili kila Mtanzania apate huduma za bima, akikazia zaidi upande wa afya.

Nae Bw. Elias Omondi Afisa Mkuu Ubunifu na Ustahimilivu FSD Africa, alisema taasisi hiyo imejikita katika kujenga na kuboresha mifumo mbalimbali ya fedha ili kukuza uchumi na TIRA

kama kiungo muhimu katika uchumi wa nchi ina nafasi kubwa ya kuendelea kuboresha maisha ya watanzania kupitia sekta ya bima itakayoweza kuwasaidia pale wanapokumbwa na majanga mbalimbali yakiwemo magonjwa.

Pia Mshauri wa Maendeleo kwa Sekta Binafsi kutoka Ubalozi wa Uingereza Tanzania, Bw. Alex Mangowi ameipongeza Mamlaka kwa ukuaji wa sekta hiyo nchini kwa kuwepo kwa ongezeko la watoa huduma, ongezeko la ulipaji wa madai, michango ya bima katika pato la taifa, thamani ya mitaji lakini pia ubakizaji wa ada nchini na kusisitiza ubunifu, na unafuu wa bidhaa ili kuendelea kuwa na soko la bima imara.

Washiriki pia walipata nafasi ya kufanya majadiliano na mawasilisho ambapo TIRA iliwakilishwa na Meneja wa Idara – Uendelazaji Soko Bw. Edgar Shao  kwa kuwasilisha mada kuhusu  'Importance of Insurance Regulatory Sanbox' pia Bw. Alex Rocky Meneja Kitengo cha Tathmini na Uchambuzi wa Takwimu  alishiriki mdahalo na kuzungumzia mambo mbalimbali yakiwemo  ushiriki wa Mamlaka katika kuunda konsotia mbalimbali kama za Kilimo, Mafuta na Gesi ambazo zinasaidia kuleta unafuu katika bima na kukuza soko.

Mkutano huo ulhudhuriwa na watendaji wakuu wa kampuni za bima, Washauri wa Bima, Mawakala wa Bima, Kampuni za Bima Mtawanyo, Benki Bima na wadau wengine muhimu.



# TIRA Yakutana na Wadau wa Bima Zanzibar Kujadili Uboreshaji wa Huduma




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imekutana na wadau wa sekta ya bima katika mkutano maalum wa kupokea maoni na mapendekezo ya kuboresha huduma za bima nchini. Mkutano huo umefanyika Februari 2i, 2025 katika Ukumbi wa Idris Abdulwakil, Kikwajuni, Zanzibar.

Katika hotuba yake kabla ya kuanza kwa majadiliano, Naibu Kamishna wa TIRA, Khadija Issa Said, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisisitiza kuwa bima ni nyenzo muhimu inayotoa kinga dhidi ya majanga, hivyo ni lazima kuhakikisha wananchi wanapata elimu sahihi kuhusu umuhimu wake.

Aliwataka wadau wa sekta ya bima kuongeza uwazi na uadilifu, hasa katika kushughulikia madai ya wateja, ili kujenga imani ya wananchi kwa sekta hiyo. Pia, aliwasihi kampuni za bima kuhakikisha wanalipa fidia kwa wakati na kwa haki.

Katika hadhara hiyo washiriki walitoa maoni kuhusu changamoto wanazokutana nazo huku wakisisitiza juu ya kupatiwa elimu kuhusu maswala ya bima ili kuweza kutatua changamoto hizo zikiwemo namna ya kufuatilia madai
Katika Mkutano huo watoa huduma za bima mbalimbali walikuwepo kujibu hoja za wateja ambao ni Kampuni za bima za Bumaco, Icealion, Shirika la bima la Zanzibar, Milembe, Heritage, CRDB, Tanzindia, Jubilee na kadhalika lakini pia alikuwepo mwakilishi wa Kampuni ya bima Mtawanyo ya Grandree.











# Mabenki Yahimizwa Kupunguza Ujira ili Gharama ya Bima iwe Rahisi



Kamishna wa Bima, Dkt. Baghayo Saqware, amewahimiza watoa huduma za bima, hususan mabenki, kupunguza ujira wanaodai kutoka kwa kampuni za bima ili kusaidia kupunguza gharama za usambazaji wa huduma hiyo. Ameyasema hayo Februari 24, 2025 katika awamu ya pili ya ziara yake inayolenga kuhamasisha utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, Kanda ya Magharibi, na Kanda ya Ziwa Tanganyika, ambapo imeanzia mkoani Shinyanga.

Lengo la ziara hiyo ni kuwaelimisha wakuu wa mikoa, makatibu tawala, na watumishi wa serikali kuhusu umuhimu wa bima, kutambulisha ofisi za kanda za TIRA na majukumu yake, pamoja na kuwaandaa kuwa mabalozi wa bima kwa wananchi wanaowahudumia.

Katika ziara hiyo, Dkt. Saqware, Wakurugenzi na Watumishi wa TIRA, walikutana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, aliyemuwakilisha Mkuu wa Mkoa, CP Salum Hamdun. Baadaye, walifanya mkutano wa kutoa elimu ya bima kwa watumishi wa mkoa, mkutano ambao ulifunguliwa na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Bw. Julius Mtatiro.

Bw. Mtatiro alisisitiza kuwa Serikali inaendelea kuboresha mifumo ya bima ili kuhakikisha wananchi wengi wananufaika, akibainisha kuwa kupitia uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Tanzania imefanikiwa kuanzisha Bima ya Afya kwa Wote. Aliwataka watumishi wa umma kuwa mstari wa mbele katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa bima.

Wakihitimisha mkutano huo, Dkt. Saqware alisisitiza kuwa kupunguza gharama za usambazaji wa bima kutawawezesha wananchi wengi kumudu huduma hizo, huku makampuni ya bima yakilipa kodi stahiki kwa serikali na kuongeza pato la taifa.















# DC Chakechake Asisitiza Ushirikiano Sekta ya Bima




Mkuu wa wilaya ya Mkoani Hamad Omar Bakar amesisitiza ushirikiano ndani ya sekta ya bima ili kukuza soko, ameyasema hayo katika mkutano wa kupokea maoni ulioandaliwa na TIRA kwa lengo la kuboresha huduma za bima nchini uliofanyika kwenye ukumbi wa Kibirinzi Chakechake Pemba, tarehe 24 Februari 2025.

Mkuu huyo wa wilaya amezitaka taasisi za bima kuwa na ushirikiano na jamii katika kutatua kero zinazowakabili ili kuimarisha huduma za bima nchini.

Aidha, aliongeza ili huduma za bima ziweze kuwa bora na kuleta ustawi na maendeleo ya jamii ni muhimu kukaa na wadau wake kuona changamoto zao zinapatiwa ufumbuzi wa kina.

Pia Naibu Kamishna wa Bima Tanzania Bi. Khadija Issa Said katika mkutano huo amewataka wadau kuwa huru katika kutoa maoni yao ili kuboresha huduma za Mamlaka hiyo na hatimae kuhakikisha inatoa huduma stahiki na kwa ufanisi Kwa jamii.

Nao baadhi ya wadau hao wameiomba Mamlaka ya Bima kuendelea kutoa msaada kwa wananchi wanapopata tatizo la kuchelewa Kwa muda mrefu kulipwa fidia Kwa mhanga , huku wakiiomba Mamlaka kuchukua juhudi za makusudi kutoa elimu juu ya umuhimu wa bima Kwa jamii.










MAMLAKA YA USIMAMIZI
WA BIMA TANZANIA
MKUTANO WA KUPOKEA MAONI
NA MAPENDEKEZO YA KUBORESHA
HUDUMA ZA BIMA NCHINI



# TIRA Yaendelea Kuhamasisha Utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote Mkoani Kigoma







Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imeendelea na ziara yake ya kutoa elimu kuhusu Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ikifika mkoani Kigoma Februari 26, 2025.


Katika ziara hiyo, Kamishna wa Bima, Dkt. Baghayo Saqware, aliambatana na baadhi ya Viongozi na watumishi wa TIRA, alikutana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma, Ndugu Hassan Rugwa, kabla ya kufanya kikao na watumishi wa wilaya na mkoa.

Watumishi hao wamehimizwa kuimarisha ushirikiano katika utoaji wa elimu ya bima kwa wananchi, kuhakikisha wanakuwa mabalozi wa bima kwa jamii wanayoihudumia, na kusaidia katika urahisishaji wa upatikanaji wa huduma za bima kwa wananchi wa Kigoma.

Dkt. Saqware alisisitiza kuwa uelewa wa bima ni msingi wa mafanikio ya utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, hivyo ni muhimu kwa viongozi wa mkoa kushiriki kikamilifu katika kuhamasisha wananchi kujiunga na huduma za bima kwa manufaa yao na maendeleo ya taifa.


Mamlaka ya
Usimamizi wa
Bima Tanzania
(TIRA)


Mamlaka y
Usimamizi wa
Tanzania (TI





# Changamkieni Fursa Muwe Mawakala wa Bima – Dkt. Saqware



Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware, amewahimiza watumishi wa Ofisi ya Mkoa wa Kagera kutumia fursa za uwekezaji katika sekta ya bima kwa kujisajili kama mawakala wa bima.

Akizungumza leo, 27 Februari 2025, katika kikao cha elimu ya bima kilicholenga kuhamasisha utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Dkt. Saqware aliwataka watumishi hao kuwa sehemu ya maendeleo ya sekta hiyo kwa kushiriki kama watumiaji wa huduma za bima na pia kuchangamkia nafasi za kuwa watoa huduma.

“Changamkieni fursa hii kwa kuwahamasisha wengine kutumia bima, hasa bima ya afya. Pia, mnaweza kutengeneza kipato cha ziada kwa kujisajili kama mawakala wa bima," alisema Dkt. Saqware.

Ziara hii ni sehemu ya jitihada za *Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) kuhakikisha uelewa wa bima unaenea kwa wananchi, huku ikitoa nafasi kwa kila mwananchi kushiriki moja kwa moja katika maendeleo ya sekta ya bima.

# TIRA, POLISI Kutumia Mifumo ya Kuimarisha Usalama Barabarani



Tarehe 3 Februari 2025, Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware, alipokea ziara fupi ya mkuu wa kikosi cha usalama barabarani Tanzania, Kamanda SACP William F. Mkonda (CO-Traffic-Tanzania), katika Ofisi ndogo za makao makuu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) zilizopo Mtendeni, Dar es Salaam.

Lengo kuu la ziara hiyo lilikuwa kujadili na kuweka mikakati ya ushirikiano baina ya TIRA na Jeshi la Polisi Tanzania katika maandalizi ya kikao kazi cha makamanda wa polisi wa usalama barabarani wa mikoa na wilaya, chenye lengo la kuweka mikakati madhubuti ya kupunguza ajali za barabarani na madhara yake kwa watumiaji wa barabara.

Kamanda Mkonda alisisitiza umuhimu wa elimu ya bima kwa makamanda wa polisi, hasa katika uhakiki wa bima kupitia mifumo rasmi. Aidha, Dkt. Saqware, alipendekeza hatua ya kuunganisha mifumo ya TIRA na Polisi ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za ajali mara moja pindi zinapotokea.

Hatua hiyo iililenga kuhakikisha waathirika wa ajali wanapata fidia zao kwa haraka, kwani taarifa za ajali zitasomwa moja kwa moja na kampuni za bima kupitia mfumo wa TIRA.

# Kateni Bima za Afya, Gharama Nafuu Matibabu Bila Kikwazo




Tarehe 12 Februari 2025 Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ilishiriki katika Kongamano la kuukaribisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan lililoandaliwa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) llilofanyika BAKWATA Makao Makuu Kinondoni, Dar es Salaam huku hadhira iliyohudhuria kongamano hilo kusisitizwa kukata bima za Afya ili kujipatia matibabu pindi wanapougua, bila ya vikwazo vya kifedha.

Kupitia Kongamano hilo Mamlaka imetoa elimu ya bima kwa ujumla na kusisitiza juu ya kila mtanzania kuchukua hatua ya kukinga kila anachokithamini vikiwemo afya na mali kupitia bima.

Akimuwakilisha Kamishna wa Bima Tanzania Bi. Hadija Maulid, Meneja Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa TIRA amesisitiza juu ya umuhimu wa kuwa na bima hususan bima ya afya kwa kuwa sasa sheria ya bima ya afya kwa wote ya mwaka 2023 imeshaanza kutekelezwa.

"Nawasihi ndugu zangu wekeni kinga kwa ajili ya afya zenu kwa kukata bima ya afya kwenye kampuni na mashirika mbalimbali yaliyosajiliwa na TIRA, Bima hizi za afya mtakazokata kwa gharama ndogo zitawasaidi nyie na familia zenu kupata matibabu bila vikwazo vya kiuchumi utakapougua kwa kuwa tayari ulishachangia awali"

Awali Naibu Kadhi Mkuu Sheikh Ally Ngeruko aliwashukuru TIRA na sekta ya bima kwa jumla kwa kuwapatia Watanzania wenye uhitaji bima za afya 1093 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Kamishna wa Bima Tanzania kutoa bima 10,000 kwa Watanzania wenye uhitaji kupitia Mufti.

Zoezi hilo linaendela kutekelezwa kwa awamu ili kuhakikisha lengo lililowekwa linatimia la kugawa bima Elfu kumi linatimia.

Katika kongamano hilo Kampuni ya Bima ya Assemble imeshiriki kutoa huduma mbalimbali za bima ikiwemo elimu na upimaji wa afya.






Idara ya Elimu Mahakama ya Kadhi Baraza kuu la Waislam Tanzania
BAKWATA
KONGAMANO LA KUKARIBISHA
MWEZI MTUKUFU WA

# TIRA Yawezesha Waandishi wa Habari Njombe Kuripoti Taarifa za Bima kwa Ufanisi





Februari 7, 2025, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ilitoa mafunzo ya jinsi ya kuripoti na kuandika taarifa za bima kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Njombe kupitia Umoja wa Njombe Press Club (NPC).

Mafunzo haya yalitolewa na wataalamu kutoka TIRA kupitia ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wakiongozwa na Meneja wa Kanda hiyo, Bi. Neema Lutula, wakishirikiana na Bw. Lucian Ndumbaro, Afisa Bima, pamoja na wawakilishi kutoka Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, Bi. Tabia Mchakama na Bw. Abubakar Kafumba.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Bi. Neema Lutula alisisitiza umuhimu wa waandishi wa habari kuwa na uelewa mpana kuhusu sekta ya bima ili waweze kuripoti kwa usahihi na weledi.

"Waandishi wa habari ni kiungo muhimu kati ya TIRA na jamii. Kupitia kalamu zenu, jamii inapata taarifa sahihi kuhusu umuhimu wa bima na jinsi inavyoweza kunufaika nayo." Alisema Bi. Neema.

Kwa upande wake, Bw. Lucian Ndumbaro alieleza kuwa mafunzo hayo pia yanatoa fursa kwa waandishi kufahamu misingi ya kisheria inayosimamia sekta ya bima pamoja na kanuni za uandishi bora wa taarifa zinazohusu bima. "Tunataka kuona taarifa za bima zikiandikwa kwa namna rahisi na inayoeleweka ili kila Mtanzania apate uelewa wa masuala ya bima," aliongeza.

Mafunzo haya ni muendelezo wa jitihada za Mamlaka ya Usimamizi wa Bima kutoa elimu kwa umma, lakini pia kuyafikia makundi mbalimbali yenye mchango mkubwa katika uenezaji wa taarifa sahihi kuhusu bima.

Matarajio yaliyoko baada ya mafunzo haya ni kuongezeka kwa ushiriki wa waandishi wa habari katika kuielimisha, kuuhabarisha, na kuhamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu bima kwa ujumla. TIRA inaamini kuwa kupitia ushirikiano huu na vyombo vya habari, uelewa wa umma kuhusu bima utaongezeka, na hivyo kuchangia katika ukuaji wa sekta ya bima nchini.



# Ukurasa wa Kamishna

UKURASA WA KAMISHNA WA BIMA

# Bima na wewe: Maswali muhimu kuhusu bima kwa Kamishna na majibu yake

Hadija Maulid,Meneja Uhusiano na Mawasiliano-TIRA

Karibu katika ukurasa rasmi wa Kamishna wa Bima, unaochapishwa kila mwezi na gazeti la Mwananchi. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa wananchi wana uelewa mpana kuhusu sekta ya bima nchini.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imeandaa toleo hili maalum likilenga kutoa majibu kwa maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu bima. KARIBU.



Kamishna wa Bima Tanzania, Dk Baghayo Saqware.

> TIRA tunahakikisha kuwa sekta ya bima inakuwa imara na inawanufaisha wananchi wote. Tunakaribisha maswali na maoni kutoka kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya bima ili kuongeza uelewa na kushughulikia changamoto zinazowakumba,"
>
> Dk Baghayo Saqware, Kamishna wa Bima Tanzania

**Bima ni nini na kwa nini ni muhimu?**

Jibu: Bima ni mfumo wa kifedha unaomwezesha mtu binafsi au taasisi kulindwa dhidi ya hasara inayoweza kutokea kutokana na majanga mbalimbali kama ajali, moto, ugonjwa, au kifo. Kwa kulipa kiasi fulani cha fedha kinachojulikana kama "premium," mteja hupata uhakika wa fidia iwapo hatari iliyobainishwa kwenye mkataba wa bima itatokea. Bima husaidia kupunguza athari za kifedha na kuboresha maisha ya watu na uchumi wa Taifa.

**Ni aina gani za bima zinazopatikana Tanzania?**

Jibu: Kuna aina kuu nne za bima ambazo ni;

Bima ya jumla (General Insurance)

Hutoa kinga dhidi ya hasara zinazotokana na ajali, moto, wizi, mafuriko, na majanga mengine yasiyotabirika.

Aina: Bima ya Magari, Bima ya Nyumba, Bima ya Biashara, Bima ya Usafirishaji.

Bima ya maisha (Life Insurance)

Hutoa fidia kwa warithi wa mteja endapo atafariki au kwa mteja mwenyewe baada ya muda uliokubaliwa.

Aina: Bima ya Maisha ya Muda, Bima ya Maisha ya Kudumu, Bima ya Maisha ya Akiba.

Bima ya Afya (Health Insurance)

Hugharamia gharama za matibabu kama hospitali, dawa, vipimo, na matibabu maalum.

Aina: Bima ya Afya ya Kibinafsi, Bima ya Afya ya Kikundi, Bima ya Afya ya Serikali.

Bima ya Takaful (Takaful Insurance)

Takaful ni mfumo wa bima wa ushirikiano unaozingatia misingi ya Shariah, ambapo wanachama huchangia fedha kwa pamoja ili kusaidiana katika kukabiliana na hasara au majanga yanayoweza kutokea.

**Je, bima ni ya lazima kwa kila mtu?**

Jibu: Baadhi ya bima ni za lazima kisheria kama vile;

Bima ya vyombo vya moto

Hii ni bima ya usafiri wa umma na binafsi ambavyo mtu hatakiwi kutumia vyombo hivyo pasipo kuwa na bima na anaweza kuhakiki kabla ya kuvitumia kupitia mfumo wa TIRAMIS .

Bima ya afya

Hii ni bima ya lazima kwa watu wote na waajiri wanatakiwa kuhakikisha kila mfanyakazi ana bima hii.

Bima nyingine za lazima ni; bima ya majengo ya biashara, bima ya public liability, bima ya masoko ya umma, bima za mizigo, bidhaa na shehena zinazoagizwa kutoka nje ya nchi na bima za vyombo vya usafiri wa majini.

Bima nyingine ni za hiari lakini zinapendekezwa kwa usalama wa kifedha wa mtu binafsi na biashara.

**Kampuni za bima zinahakikisha vipi kuwa zina uwezo wa kulipa madai?**

Jibu: TIRA inasimamia na kuhakikisha kuwa kampuni zote za bima zina akiba ya kutosha kulipa madai ya wateja wao. Pia, tuna mifumo ya ukaguzi wa fedha inayozuia kampuni zinazoendeshwa kwa uzembe na zisizo na uwezo wa kifedha.

**Nifanye nini kuchagua bima sahihi?**

Jibu: Zingatia yafuatayo:

Fahamu mahitaji yako na aina ya kinga unayohitaji, angalia kampuni za bima zilizosajiliwa na TIRA na soma masharti na vigezo vya mkataba wa bima kabla ya kujiunga.

**Je, kuna bima za wakulima?**

Jibu: Ndiyo. Kuna bima ya kilimo inayolinda wakulima dhidi ya majanga kama ukame, mafuriko, au magonjwa ya mazao.

**Je, bima inaweza kurudisha pesa yangu kama sijapata tatizo?**

Jibu: Kwa kawaida, ada ya bima hairejeshwi ikiwa hatari iliyokingwa haikutokea, isipokuwa kwa baadhi ya bima maalum zinazorudisha sehemu ya michango.

**Madai ya bima yanachukua muda gani kulipwa?**

Jibu : Endapo nyaraka zote zinazohitajika zimewasilishwa, madai yanapaswa kushughulikiwa ndani ya siku 45 kwa mujibu wa kanuni za TIRA.

**Je, TIRA inatoa msaada gani kwa wateja waliopunjwa na kampuni za bima?**

Jibu: TIRA ina dawati maalum la kushughulikia malalamiko ya wateja na kuhakikisha kuwa haki inatendeka.

**Je, ninaweza kuwa na zaidi ya bima moja?**

Jibu: Ndiyo. Unaweza kuwa na bima zaidi ya moja kulingana na mahitaji yako.

**Je, kampuni za bima zinaweza kukataa kulipa madai yangu?**

Jibu: Kampuni za bima zinaweza kukataa kulipa madai ikiwa mteja hajatimiza masharti ya mkataba, kama vile kutoa taarifa za uongo au kushindwa kulipa ada ya bima kwa wakati.

**Bima ya afya inafanya kazi vipi?**

Jibu: Bima ya afya huwezesha kupata huduma za matibabu kwa gharama nafuu, ambapo kampuni ya bima hulipa sehemu au gharama zote kulingana na mkataba.

**Bima ya maisha ina faida gani kwa familia yangu?**

Jibu: Bima ya maisha huwapa wategemezi wako msaada wa kifedha endapo utafariki dunia, ikiwasaidia kulipa gharama za mazishi, elimu ya watoto, na gharama nyingine muhimu.

**Je, kuna bima ya mikopo kwa wajasiriamali?**

Jibu : Ndiyo. Bima ya mikopo inamlinda mkopaji na familia yake dhidi ya athari za kushindwa kulipa mkopo endapo atafariki dunia au kushindwa kufanya kazi.

**Je, sekta ya bima inachangia je uchumi wa Tanzania?**

Jibu: Sekta ya bima inachangia ukuaji wa uchumi kwa kutoa ajira, kusaidia biashara na miradi mikubwa, na kulinda wawekezaji dhidi ya majanga ya kifedha.

**Je, TIRA ina mfumo wa kidigitali wa kusimamia sekta ya bima?**

Jibu : Ndiyo. TIRA ina mifumo ya kidigitali inayosaidia katika usimamizi wa madai, utoaji wa leseni, na upatikanaji wa taarifa kwa umma kwa uwazi zaidi.

**Je, ni kweli kuwa bima ni kwa matajiri tu?**

Jibu: Hapana. Bima ni kwa kila mtu, na kuna bima za gharama nafuu zinazokidhi mahitaji ya watu wa kipato cha chini na cha kati.

TIRA inahakikisha kuwa sekta ya bima inakuwa imara na inawanufaisha wananchi wote. Tunakaribisha maswali na maoni kutoka kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya bima ili kuongeza uelewa na kushughulikia changamoto zinazowakumba.

Tunawahimiza Watanzania wote kujifunza zaidi kuhusu bima na kuchukua hatua sahihi za kujilinda kifedha kwa mustakabali bora.

**Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania**
**JENGO LA PSSSF, Ghorofa ya 5, Mtaa wa Makole,S.L.P 2987, DODOMA, Tanzania,**
**Barua pepe : coi@tira.go.tz | Simu/Nukushi**
**Piga Bure: +255 26 2321180 | Simu: +255 0222135137 | Nukushi: +255 26 2321180**

*Kama una mada yoyote inayohusu bima unataka iandikwe katika ukurasa huu kwa lengo la kuelimisha jamii usisite kuwasiliana nasi kupitia anuani yetu maoni@tira.go.tz tuma ujumbe kupitia Na. ya simu 0739 525444*
*TIRA: Kwa Soko Salama la Bima*

MCL "Epaper Copy"

# Matukio kwenye Vibango




Mamlaka ya Usimamizi
wa Bima Tanzania (TIRA)
UWASILISHAJI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA SOKO LA BIMA TANZANIA 2023/24
20 Februari 2025
Kuanzia Saa 2:00 asubuhi
Hotel Verde, Zanzibar
MGENI RASMI:
Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
TIRA Kwa Soko Salama la Bima
Karibuni
coi@tira.go.tz
www.tira.go.tz
+255 222 132 537
FB, IG, X: //@tira_tz


MAMLAKA YA USIMAMIZI
WA BIMA TANZANIA (TIRA)
Mafunzo kwa wajumbe wa Bodi ya Taifa ya Bima
Ukumbi wa ZURA Zanzibar 19 Feb 2025
Kupitia mafunzo haya tunapata fursa ya kujifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu maendeleo na utatuzi wa changamoto katika sekta ya bima
Dkt. Suleiman R. Mohamed
Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Bima
+255 022 213 2537
coi@tira.go.tz
www.tira.go.tz
tira_tz


Mamlaka ya Usimamizi
wa Bima Tanzania (TIRA)
Heri ya Siku ya
Kuzaliwa
Bi. Khadija Said
Naibu Kamishna wa Bima Tanzania
Tunakutakia afya njema, furaha tele na mafanikio.
Tunauthamini mchango wako katika kukuza na kuendeleza sekta ya bima nchini.
coi@tira.go.tz
www.tira.go.tz
+255 222 132 537
FB, IG, X: //@tira_tz


MAMLAKA YA USIMAMIZI
WA BIMA TANZANIA (TIRA)
TIRA
Updates
Bi. Emmy K. Hudson
Mjumbe Bodi ya Taifa ya Bima
Bi. Emmy K. Hudson, Mjumbe Bodi ya Taifa ya Bima, akitoa maoni katika wasilisho kuhusu Skimu ya Bima ya Kilimo (TAIS) katika Mafunzo ya kwa Wajumbe hao.
Mafunzo kwa wajumbe wa Bodi ya Taifa ya Bima
Ukumbi wa ZURA Zanzibar 19 Feb 2025
+255 022 213 2537
coi@tira.go.tz
www.tira.go.tz
tira_tz


Mamlaka ya Usimamizi
wa Bima Tanzania (TIRA)
UWASILISHAJI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA SOKO LA BIMA TANZANIA 2023/24
1
BADO SIKU
20 Februari 2025
Kuanzia Saa 2:00 asubuhi
Hotel Verde, Zanzibar
coi@tira.go.tz
www.tira.go.tz
+255 222 132 537
FB, IG, X: //@tira_tz


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Fedha
Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)
KHERI YA SIKU YA KUZALIWA
Balozi wetu wa Bima Mhe. Wanu Hafidh Ameir.
Tunakushukuru kwa ushirikiano wako katika kuendeleza sekta ya Bima nchini. Tunakuombea afya njema na maisha marefu zaidi
FEBRUARI
27
TIRA KWA SOKO SALAMA LA BIMA
@tira_tz
www.tira.go.tz



# TIRA & 2025


**Mamlaka ya Usimamizi wa Bima**
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
PSSSF HOUSE, 5th Floor, Makole Street, P.O. Box 2987
DODOMA, Tanzania.

coi@tira.go.tz
+255 26 2321180
+255 0222135137
+255 26 2321180

**FB, IG, X:** //@tira_tz
www.tira.go.tz